# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## SHULE YA SEKONDARI MATOMBO

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO 2025

**Toleo la:**
**Mei, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO**

Mkuu wa Shule
Shule ya Sekondari Matombo,
S.L.P 749,
**MOROGORO**.

Simu:
Mkuu wa shule: 0714 907 572
Makamu mkuu wa Shule: 065518292
Mwandamizi Taaluma: 0654814768

---

Unapojibu tafadhali taja

**Kumb.Na.MHS/JIns-025/BTCH-09**

**MZAZI WA______________________________________**

**S.L.P ________________________________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO MKOA WA MOROGORO MWAKA2025/26.**

Tafadhali husika na mada hapo juu ambayo ni kicho cha barua hii.

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya sekondari Matombo mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya HGL/HKL/HGLi/HGfa/HGK (Kata isiyohusika)

Shule ya Sekondari MATOMBO ipo umbali wa Kilometa 64 Kusini-Mashariki mwa Mji wa Morogoro. Usafiri wa basi kutoka mjini Morogoro unapatikana katika kituo cha mabasi mafiga au Karoleni ambapo nauli ni Shilingi 8,000/= na shuka kituo kinachoitwa Msalabani (ikiwa utapanda gari Kituo cha Mafiga zinazoelekea Kisaki au shukia stendi ya Matombo ndani (ikiwa utapanda gari Kituo cha Karoleni zinazoelekea Tawa).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 07/07/2025, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 05/07/2025 Mwisho wakuripoti ni tarehe 20/07/2025.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

### 1.1 Sare za Shule

Sare ya shule hii ni:

1. Sketi ndefu mbili (02) rangi ya DARK BLUU. (kitambaa cha ubora wa gredi one), Mshono - isiyobana mwili yenye Linda box kubwa. (Tazama picha katika kiambatisho cha sare za shule hii) Au njoo Tsh 25,000/= kwa kuwa zinapatikana duka lilopo karibu na shule.
2. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yakiwa na nembo ya shule ya sekondari MATOMBO. Au anaweza kuzipata kwenye duka lililopo karibu na shule kwa gharama ya Tsh 12,000 (kwa shati moja).
3. Aje na hijab (kijuba) ya shule ya rangi nyeupe na ya Kushindia ya rangi ya blue zote zifunike kifua cha mwanafunzi pia ziwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. Au anaweza kuzipata kwenye duka lililopo karibu na shule kwa gharama ya Tsh 15,000/- kwa kila moja.
4. Track suit ikiwa na nembo ya shule ya sekondari Matombo, namba ya utambulisho wa mwanafunzi ya rangi ya dark bluu au TSH 30,000/= kwa kuwa zinapatikana katika duka lililo karibu na shule ikiwa ina nembo na chapa nyinginezo.
5. Aje na T-shirt rangi ya bluu bahari (FORM SIX) zienye nembo ya shule ya sekondari Matombo au zinazopatikana shuleni zikiwa na nembo ya shule kwa Tsh 12,000/-
6. Aje na Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; (Buti, travota, sneekers ahaziruhusiwi kuziruhusiwi shuleni kama viatu vya shule)-kiambatisho kimewekwa. Pia aje n araba kwa ajili ya michezo.
7. Aje na Soksi jozi mbili nyeupe;
8. Sweta moja au mawili rangi ya dark bluu (Sweta lolote la nyumbani halitakiwi.
9. Aje na nguo ya kushindia sketi mbili za rinda box zenye viboksi vya dark blue ndefu yenye kunika vifundo vya miguu. AU anaweza kuzipata kwenye duka la karibu na shule kwa gharama ya TSH 20,000/=

**MUHIMU: Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa Sare iliyo tofauti katika rangi, mshono, nembo na kipimo kinyume na maelekezo yaliyopo kwenye fomu hii. Aidha (Shati la shule, tshirt na Track suit ni lazima ziwe na nembo ya shule kwa kuzingatia fomu hii ya maelekezo).**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**
Madaftari ya kaunta book tisa au zaidi Q 3.

1. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka na rulled paper (karatasi za mistari mbili (02) kwa mwaka; Zinatolewa kwa awamu kwa mihula miwili. (RIMU INAPATIKANA KWENYE DUKA KARIBU NA SHULENI KWA TSH 12,000/= TU na RULED PAPER INAPATIKANA KWA TSH 8,000 TU.)
2. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*wasiliana na Mwalimu wa taaluma ikiwa utahitaji msaada zaidi.*);
3. Godoro lenye vipimo vya 2.5x6
4. Shuka za rangi ya pinki Jozi2, blanket 1, mto na foronya ya mto, chandarua1 cheupe; Nguo za ndani za kutosha Pamoja na kanga, kitenge na taulo.
5. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
6. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
7. Mwanafunzi wa Tahasusi ya HGL na HKL waje na vifaa vifuatavyo vya usafi:

| *KIFAA* | *SOFT BROOM* | *FAGIO CHEREWA* | *TOILET BRUSH* | *RUBBER OR SQUEZER* | *JEMBE&MPIN I* | *LIQUID SOAP* | HARD BROOM |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *IDADI* | *1* | *1* | *1* | *1* | *1* | *1 LT* | *1* |

na wanafunzi wa Tahasusi ya **HGLi ,HGFa** na **HGK** waje na vifaa vifuatavyo vya usafi:

| *KIFAA* | *SLASHER* | *RAKE* | *KIZOLEO* | *BUCKET 20L* | *LIQUID SOAP* |
|---|---|---|---|---|---|
| *IDADI* | *1* | *1* | *1* | *1* | *3 LT* |

8. Folder File moja la kutunzia nyaraka muhimu za mwanafunzi.
9. Picha ya passport size mbili za mwanafunzi na moja kwa kila mzazi/mlezi wa karibu atakayejazwa kwenye fomu ya taarifa za wazazi/walezi.

### Michango mbalimbali

Shule ya Sekondari MATOMBO ni ya Bweni, hivyo mwanafunzi unatakiwa kuweka michango ifuatavyo kwenye akaunti ya shule kabla ya kuripoti shuleni na ufike na risiti ya benki au risisti ya kielekriniki kuthibitisha malipo yako.

| **Na** | **Aina yaMchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo yafanyike kupitia akaunti namba **22101100129** Jina **MATOMBO SECONDARY SCHOOL self reliance** Benki ya **NMB**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
3. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
9. Kutunza mali za shule;
10. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
11. Mwanafunzi haruhusi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
12. radio, pasi ya umeme pia haviruhusiwi.

## MUHIMU:

1. **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi mwanfunzi atawasiliana na ndugu, jamaa na walezi wake kwa idhini ya mkuu wa shule kupitia walimu au watumishi kwa namba zilizoidhinishwa na shule tu.**

2. **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Nimarufuku mwanafunzi kulala kitanda**

**kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

3. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (sababu msiba wa watu wa karibu au ugonjwa**).

A. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA NI PAMOJA NA:**

a) Wizi;
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
c) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
e) Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
f) Kusuka nywele kwa msuko wowote. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
g) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya; kama Uvutaji wa sigara, bangi na kadhalika.
h) Uasherati,mahusiano ya jinsia moja,kuoa au kuolewa;
i) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
j) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
k) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
l) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule bila kufuata utaratibu uliwekwa na shule;
m) Kudharau Bendera yaTaifa;
n) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
o) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

- Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
- Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
- Picha ya passport size1 ya kila mzazi au ndugu wa karibu wa mwanafunzi wasiozidi 04 wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu.
- Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
- Mwanafunzi aje na nakala ya hati ya matokeo (result slip) ya kidato cha nne pamoja na ya cheti cha kuzaliwa.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATOMBO**

**MARIAM R. MADAMBA**

**MKUU WASHULE**

THE HEADMISTRESS
MATOMBO SEC. SCHOOL
P. O. B0x 749
MOROGORO

**ZINGATIA:**

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**Mkuu wa shule 0714907572**
**Makamu Mkuu wa Shule 0655182992**
**Mwandamizi Malezi 0741879879**

**Aidha wakati wa kuripoti shule itakupatia namba maalumu za mawasiliano za shule ambazo zinatumika kupokea fedha na mawasiliano ya wanafunzi wawapo shuleni. Namba hizo pekee ndizo zitatumika katika mawasiliano yaliyo rasmi kati ya mzazi na mwanafunzi.**

MATOMBO SEC SHOOL,
P O BOX 6169,
**MOROGORO**.

Ref.No.............................................

**PART A: -**

To the Medical Officer,
........................................................
........................................................
........................................................

**REF:**

**.....................................................................................................................................**
**...........................**

Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a girl for Secondary Schools' education.

1. a. Eyesight
   b. Hearing
   c. Limbs
   d. speech
   e. venereal
   f. disease
   g. Leprosy
   h. Epilepsy I. Neurosis
   Other diseases
   like pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**)
I have examined the above-named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

a). Eyesight......................................

b). Hearing.......................................

c). Limbs ......................................

d). Speech.......................................

e). Venereal diseases ....................

f). Leprosy...................................

g). Epilepsy..................................

h). Neurosis.................................

i). Other serious diseases........................
Pregnancy...........................

Name..........................................................
Signature..........................                Date..........................
**STATION**.............................................................
**DESINATION**..................................................
**N.B.,** I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.

**FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1.JINA LA MWANAFUNZI.............................................................................................

2.JINA LA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI....................................................................

3.JINA LA SHULE ANAKOTOKA...........................................................................................

4.TAREHE YA KUZALIWA..............................................................................................

5.KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI..................................................................................

6.WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI...............................................................................

7.MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI...................................................................................

8.KABILA.................................................................................................................

9.URAIA......................................................................................................................

10.DINI/DHEHEBU........................................................................................................

11.ANUANI YA MZAZI/MLEZI..............................................................................................

NAMBA YA SIMUYA MZAZI/MLEZI. -NYUMBANI..............................................

-OFISINI....................................................

NAMBA YA WHATSAPP KWA AJILI KUTUMA MATOKEO: (Inaweza kuwa ya ndugu wa karibu)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

MAJINA MANNE YA NDUGU WAKARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARURA ITATOKEA: -

| **Na** | **JINA** | **UHUSIANO** | **ANAKOISHI** | **NAMBAY A SIMU** |
|---|---|---|---|---|
| 01. | | | | |
| 02. | | | | |
| 03. | | | | |
| 04. | | | | |

## VIELELEZO VYA SARE ZA SHULE NA VIATU VINAVYOTAKIWA



SKETI YA SHULE NA TSHIRT



SHAMBA DRESS



TRACK SUIT ZA MICHEZO

**KIELELEZO CHA VIATU VINAVYORUHUSIWA NA VISIVYORUHUSIWA**

